

MINUTE SHEETS

Dokezo No.

Kumb. Na. TAFIRI/HQ/W.I/Vol. IV/119

WATUMISHI WOTE TAFIRI

Yah: **UWASILISHAJI WA MICHANGO YA PENSHENI KATIKA
MFUKO WA PENSHENI KWA WATUMISHI WA UMMA
(PSSSF) KWA WALIOKUWA WANACHAMA WA MFUKO WA
TAIFA WA HIFADHI YA JAMII (NSSF)**

Husika na kichwa cha habari hapo juu.

1. Kutokana na maelekezo yaliyotolewa na Serikali pamoja na Chama cha Waajiri Tanzania (TAE), Waajiriwa katika Sekta ya Umma ambao walikuwa wanachangia katika Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii nchini (NSSF), watapaswa kuchangia katika Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF). Jumla ya mchango utakaowasilishwa ni asilimia 20 ukichangiwa kati ya mtumishi kukatwa katika mshahara (5%) na Mwajiri kumchangia pia (15%).
2. Uwasilishaji wa michango husika ulitakiwa kuanza tangu Mwezi Februari, 2019. Hivyo, michango iliyowasilishwa NSSF kuanzia Februari, 2019 itawasilishwa PSSSF.
3. Ikiwa kuna kipindi chochote ambacho mtumishi anadaiwa na NSSF kuanzia mwezi Januari 2019 kurudi nyuma, michango husika itapaswa kulipwa NSSF. Hivyo, mnshauriwa kuangalia "contribution summary report" ili kujiridhisha kuwa hakuna michango ambayo haikuwasilishwa kipindi cha kuanzia mwezi Januari, 2019 kurudi nyuma. Aidha, miezi iliyochangiwa katika Mfuko wa NSSF italindwa kisheria wakati wa kulipa mafao ya watumishi husika.

